

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**SERIKALI YATAIFISHA MADINI YA ALMASI YALIYOKAMATWA UWANJA WA NDEGE
WA DAR ES SALAAM**

Serikali imetaifisha madini ya Almasi yaliyokamatwa Agosti 31, mwaka huu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam baada ya kubainika kuwepo udanganyifu mkubwa wa thamani halisi ya madini hayo uliofanywa na wasafirishaji

Agizo la kuitaifisha almasi hiyo limetolewa na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb), mara baada ya kupokea ripoti ya usafirishwaji wa madini hayo, pamoja na kuukagua mzigo huo.

Dkt. Mpango amesema endapo mzigo huo ungesafirishwa kwenda nje ya nchi, nchini Ubelgiji na Kampuni ya madini ya Williamson Diamond Ltd, Taifa lingeingia hasara ya mabilioni ya fedha kwani palikuwa na udanganyifu mkubwa katika ukokotozi wa hesabu zake, hasa gharama yake pamoja na gawio halisi la serikali.

"Walisema thamani ya almasi iliyokamatwa ni dola milioni 14.798, sawa na Shilingi bilioni 33 wakati wataalamu wamebaini almasi ile ilikuwa na thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 29.5 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 65..... Zilibaki dakika 5 tu ndege iondoke na kama si watendaji wazalendo tungebiwa hizi almasi" alisema Dkt. Mpango.

Waziri huyo wa fedha mbali na kumpongeza Prof. Abdulkarim Mruma ambaye ndiye aliyeweza serikali kufahamu ukweli kuhusu mzigo huo, amempa agizo kuhusu gawio la serikali la mwaka huu kutoka katika Mgodi wa Almasi wa Mwadui, baada ya kipindi chote mgodi huo kutangaza hasara kwenye biashara ya vito hivyo wakati haikuwa kweli.

"Prof. Mruma, waambie wenzako wa bodi ya Mwaui, mwaka huu tunataka gawio letu na hatutaki makombo"

Dkt. Mpango mbali na kuagiza sheria zifuatwe kutaifisha mzigo huo, ameviagiza vyombo vya dola kuwasaka na kuwakamata watendaji wote waliohusika kutoa taarifa za uongo kuhusu uzito na thamani ya Almasi hiyo na na kuwachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali zao ikibainika haziendani na kipato chao.

Pia ameagiza kuwepo kwa wataalam wa kutosha wa kufanya tathmini ya madini ya vito ndani ya miezi 6 hadi 7 katika migodi yote ili serikali iweze kupata gawio stahiki huku akiagiza upimaji wa madini uanzie migodini na vifaa vya upimaji vinunuliwe mara moja.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Prof. Abdulkarim Mruma ameitaka serikali kuwachukulia hatua watu wote waliohusika katika kuusafirisha mzigo huo, huku akishauri uwepo wa uwakilishi wa serikali katika hatua zote za mauzo ya almasi nchini na nje ya nchi.

Prof. Abdulkarim Mruma amesema pamoja na kubaini upotevu mkubwa wa fedha, kuna dosari nyingine zikiwemo kukosekana kwa vifaa ya kupimia madini hayo, almasi kusafirishwa na kuuzwa sokoni bila uwepo wa mwakilishi wa Serikali na ameshauri hatua za udhibiti huo zifanyike katika madini yote yanayochimbwa hapa nchini.

Viongozi waliokuwepo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere wakati wa kukagua madini hayo ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bw. Charles Kichere, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Bw. Biswalo Mganga, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Brigedia Jenerali John Julius Mbungo, Kamishna wa Madini Tanzania Mhandisi Benjamin Mchwampaka na Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam SACP - Lazaro Mambosasa.

Imetolewa na:

Benny Mwaipaja

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO